# KIBABII UNIVERSITY COLLEGE

## UNIVERSITY EXAMINATIONS

## 2014/2015 ACADEMIC YEAR
## FIRST YEAR SECOND SEMESTER

## MAIN EXAMINATION

## FOR THE DEGREE OF MASTER OF EDUCATION IN KISWAHILI

**COURSE CODE:** **LEK 800**

**COURSE TITLE:** **TEACHING KISWAHILI AS A SECOND LANGUAGE I**

**DATE:** **TIME:**

---

MAELEKEZO

Jibu maswali **matatu** pekee.

**MUDA: Masaa Matatu (3)**

**KIBUCO** observes **ZERO** tolerance to examinations cheating

**Maswali**

1. a. Kwa kutumia mifano mwafaka, fafanua dhana ya lugha, (alama 4).
   b. Dadavua sifa zozote nne za lugha huku ukirejelea lugha ya Kiswahili. (alama 16).

2. Kwa kurejelea nadharia zozote tatu, eleza michakato mbalimbali ya upataji wa Kiswahili kama lugha ya kwanza. (alama 20)

3. "Ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili unaweza kuelekezwa na maoni ya akina Naomy Chomsky na Jean Piaget." Thibitisha. (alama 20)

4. "Kiswahili kama lugha ya pili inaweza kufundishwa kwa kutumia mbinu mbalimbali." Tetea kauli hii kwa kurejelea mbinu zozote nne. (alama 20)

5. "Utafiti wa lugha ya Kiswahili umeathiri ufundishaji wake kwa namna hasi na chanya." Pambanua kauli hii kwa kutumia hoja zozote nne. (alama 20)

**KIBABII UNIVERSITY COLLEGE**

*(A Constituent College of Masinde Muliro University of Science and Technology)*

Tel: 020-2028660 / 0708-085934 / 0734-831729
P.O. Box 1699-50200
Bungoma
Kenya

E-mail: enquiries@kibabiiuniversity.ac.ke
Website: http://www.kibabiiuniversity.ac.ke


# LEK 800: TEACHING KISWAHILI AS A SECOND LANGUAGE I


**Mhadhiri: Dkt. F. C. N. S. Wanjala**

**Simu Tamba: +254726335079**

**Barua Pepe: simiyu57@yahoo.com**


## Utangulizi wa Kozi

Kozi hii inanuia kumtayarisha mwanafunzi kufundisha lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili katika shule za upili na vyuo nchini Kenya. Ni kozi ambayo inadhamiria kutoa elimu, ujuzi na maarifa mapya, mabadiliko na changamoto katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili hasa kwa kuoanisha na malengo yaliyomo katika mtaala wa elimu wa Kenya.

## Malengo ya Kozi

Kozi hii inalenga kupambanua mambo yafuatayo:

- Maana na sifa za lugha.
- Nadharia za upataji lugha.
- Nadharia za ujifunzaji lugha.
- Mbinu za kujifunza na kufundisha lugha ya Kiswahili.
- Nafasi ya utafiti katika ujifunzaji na ufundishaji wa lugha ya Kiswahili.

## Matokeo ya Ujifunzaji

Kufikia mwisho wa kozi hii, kila mwanafunzi aweze:

- Kupambanua maana na sifa za lugha.
- Kufafanua nadharia za upataji lugha.
- Kueleza nadharia za ujifunzaji lugha.
- Kubainisha mbinu za kujifunza na kufundisha lugha ya Kiswahili.

- Kutathmini nafsi ya utafiti katika ujifunzaji na ufundishaji wa lugha ya Kiswahili.

**Mawanda ya Kozi**

**Mada ya 1. Lugha na muktadha wake katika ufundishaji wa Kiswahili**

- Maana ya lugha
- Sifa za lugha
- Sifa za mwalimu wa Kiswahili

**Mada ya 2: Nadharia za upataji na ujifunzaji wa lugha**

- Nadharia za upataji wa lugha ya kwanza
- Nadharia za ujifunzaji wa lugha ya pili
- Mbinu za ufundishaji wa lugha ya pili

**Mada ya 3: Utafiti wa lugha nchini Kenya**

- Maana ya utafiti wa lugha
- Athari za utafiti katika ufundishaji wa Kiswahili
- Athari za utafiti katika ujifunzaji wa Kiswahili
- Ufundishaji wa lugha ya pili darasani
- Ufasaha na usahihi katika ufundishaji wa Kiswahili

**Tathmini ya kozi**

- Kazi-mradi (utafiti na uwasilishaji) = 40%
- Mtihani wa mwisho wa semista = 60%

**Mbinu za Ufundishaji**

Mhadhiri ataeleza kwa ujumla vipingele vyote vya kozi kupitia mbinu ya mhadhara. Kisha, wanafunzi watapewa mada mbalimbali ili wazifanyie utafiti wa kina na kuwasilisha matokeo darasani. Kwa hivyo, mbinu zitakazotumiwa kufundisha kozi hii ni pamoja na mihadhara, mawasilisho na mijadala.

## MAREJELEO


Brown, H. D. (1994). *Principles of Language Learning and Teaching* (Toleo 3.). Englewood Cliffs, New Jersey: Printice Hall Regents.

Ipara, O. I. (2002). "The Future of Kiswahili Classroom Research," katika Simala, K. I. (Mh.) Utafiti *wa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press.

Ligami. P. (2002).Ujuzi na Utendaji katika Lugha ya Pili: Umuhimu wa Utafiti, katika Simala, K. I. (Mh.). *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press.

Markey, W. F. (1965). *Language Teaching Analysis*. London: Longman.

Mbunda, F. (1976). *Mwalimu wa Lugha: Kiiswahili*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Musau, P. na L. Chacha. (2001). *Mbinu za Kufundishia Kiswahili kwa Walimu wa Shule za Msingi, Upili na Vyuo*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Nduguru, S. (1986). *Kanuni na Mbinu za Kufundisha*. Dar es Salaam: Mbogo International Graphic Arts.

Parrott, M. (1993). *Tasks for Language Teachers: A Resource Book for Training and Development*. Cambridge: Cambridge University Press.

Pearson, H. (1981). *The Teaching of Language Skills: Listening, Talking, Reading and Writing*. Nairobi: Oxford University Press.

Syambo, B. na wengine. (1987). *Jinsi ya Kufundisha Kiswahili katika Shule za Msingi*. Nairobi: Heinemann Kenya.

Tuntufye, N. D. (1972). *Jinsi ya Kufundisha Kiswahili*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House Ltd.

Wanjala, S. F. na J. M. Kavoi. (2012). *Stadi za Mawasiliano na Mbinu za Kufundishia Kiswahili*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Whitely, W. (1970). *Swahili: The Rise of a National Language*. Oxford: Oxford University Press.